COLORADO
Family and Medical Leave Insurance Program (FAMLI)
Department of Labor and Employment

# Ilani ya Mpango wa 2023 FAMLI

## Makato kutoka kwenye mishahara ya Waajiriwa yataanza kutekelezwa tarehe 1 Januari, 2023

- Mgao wa mwajiriwa wa ada za FAMLI umwekwa kuwa asilimia 0.45 ya mishahara ya waajiriwa hadi 2024. Kwa mwaka wa 2025 na zaidi, mkurugenzi wa Kitengo cha FAMLI anaweka kiwango cha ada kulingana na fomula kutegemea thamani ya pesa ya kila mwaka. Waajiri walio na jumla ya waajiriwa kumi au zaidi katika taifa zima lazima pia wachangie nyongeza ya asilimia 0.45 ya mishahara kwa jumla ya asilimia 0.9 lakini waajiri walio na waajiriwa tisa au wachache wanawajibika tu kutuma mgao wa waajiriwa wa asilimia 0.45 kwenye Kitengo cha FAMLI.
- Kuanzia mwaka wa 2023, waajiri wanaweza kuanza kukata hadi asilimia 0.45 kwenye mishahara ya waajiriwa kwa ajili ya michango ya FAMLI. Hatua hii inaweza kufanywa kupitia makato rahisi ya mishahara na waajiriwa watatambua makato kwenye hundi zao za malipo ya kawaida. Waajiri wanawajibika kukusanya makato hayo na kuyatuma kwenye Kitengo cha FAMLI kwa niaba ya waajiriwa wao mara moja kila robo mwaka.

## Fidia zitaanza kutekelezwa tarehe 1 Januari, 2024

- Kuanzia 2024, fidia za likizo ya familia na ya matibabu inayolipiwa zinapatikana kwa waajiriwa wengi wa Colorado ambao wana hali inayostahiki na waliopata dola 2,500 mwaka uliopita kwa kazi waliyofanya Colorado.
- Hali zinazostahiki likizo ya familia na matibabu inayolipiwa ni:
  - Kumtunza mtoto wakati wa mwaka wa kwanza baada ya kuzaliwa, kuasili, au uwekwaji katika huduma ya malezi ya mtoto huyo.
  - Kumtunza mwanafamilia aliye na maradhi mabaya.
  - Kutunza maradhi mabaya uliyo nayo.
  - Kuweka mipango ya mwanajeshi wa familia kutumwa mahali.
  - Kupata nyumba salama, utunzaji na/au usaidizi wa kisheria kukabiliana na dhuluma za nyumbani, kunyemelea, unyanyasaji wa kijinsia, au kudhulumiwa kingono.
- Waajiriwa wanaofidiwa wana haki ya hadi wiki 12 za likizo ya familia na matibabu inayolipiwa kwa mwaka. Watu walio na maradhi mabaya yaliyosababishwa na matatizo ya ujauzito au ya kujifungua wana haki ya hadi wiki 4 zaidi za likizo ya familia na matibabu inayolipiwa kwa mwaka kwa jumla ya wiki 16.
- Likizo inaweza kuchukuliwa mfululizo, kwa vipindi au kwa ratiba iliyopunguzwa.
- Likizo italipiwa kwa kiwango cha hadi asilimia 90 ya mshahara wastani wa kila wiki wa mwajiriwa, kulingana na kipimo kinachobadilika. Waajiriwa wanaweza kukadiria fidia zao kwa kutumia kikokotozi cha fidia kinachopatikana kwenye famli.colorado.gov.
- Si lazima umfanyie kazi mwajiri wako muda wa chini zaidi ili ustahiki fidia za likizo ya familia na matibabu inayolipiwa.
- Ikiwa likizo ya FAMLI inatumiwa kwa sababu ambayo pia inastahiki kuwa likizo kulingana na FMLA ya serikali kuu, basi likizo pia itachukuliwa kuwa likizo ya FMLA iliyotumika.
- Waajiriwa wanaweza kuamua kutumia likizo ya ugonjwa au muda mwingine wa mapumziko unaolipiwa kabla ya kutumia fidia za FAMLI, lakini hawahitajiki kufanya hivyo.
- Waajiri na waajiriwa wanaweza kukubaliana kujaliza fidia za FAMLI kwa likizo ya ugonjwa au muda mwingine wa mapumziko unaolipiwa kutoa ubadilishaji wa mshahara mzima.

## Kuwasilisha Madai

- Waajiriwa hataweza kuwasilisha madai ya fidia hadi robo ya mwisho ya 2023. Fidia zitapatikana kuanzia Januari 2024. Maagizo kuhusu jinsi ya kutuma ombi la madai yatapatikana kwenye famli.colorado.gov katika robo ya mwisho ya 2023.
- Waajiriwa au wawakilishi wao walioteuliwa wanatuma ombi la fidia za FAMLI kwa kuwasilisha ombi, pamoja na nyaraka zinazohitajika kwenye kitengo cha FAMLI moja kwa moja. Waajiri hawawezi kuwashurutisha waajiriwa kutuma ombi la fidia za FAMLI.
- Maombi yanaweza kuwasilishwa mapema kabla ya kutokuwepo kazini na wakati mwingine, yanaweza kuwasilishwa baada ya kutokuwepo kazini kuanza.
- Maombi yaliyoidhinishwa yatalipwa na Kitengo cha FAMLI ndani ya wiki mbili baada ya dai kuwasilishwa ipasavyo na kila baada ya wiki bili baadaye kwa muda wa likizo iliyoidhinishwa.
- Waajiriwa wanaweza kukata rufaa ya maamuzi ya dai kwenye Kitengo cha FAMLI.
- Watu wanaojaribu kulaghai mpango wa FAMLI wanaweza kuzuiwa kupokea fidia.

## Usalama wa kazi na fidia endelevu

- Lazima waajiri wadumishe fidia za afya kwa waajiriwa wakati wakiwa kwenye likizo ya FAMLI na mwajiri na mwajiriwa kuwajibika kulipia fidia hizo kwa viwango sawa kabla ya likizo kuanza.
- Mwajiriwa ambaye amewahi kumfanyia kazi mwajiri kwa angalau siku 180 ana haki ya kurudi katika nafasi ile ile, au nafasi sawa, anaporudi kutoka kwenye likizo ya FAMLI.

## Ulipizaji Kisasi, Ubaguzi na Usumbufu Uliopiga Marufuku

- Waajiri hawapaswi kuingilia haki za waajiriwa kulingana na FAMLI na hawapaswi kubagua wala kulipiza kisasi dhidi yao kwa kutekeleza haki hizo.
- Waajiriwa ambao watashuhudia ulipizaji kisasi, ubaguzi au usumbufu wanaweza kuwasilisha kesi mahakamani, au wanaweza kuwasilisha malalamishi kwenye Kitengo cha FAMLI.

## Taarifa Nyingine Muhimu

- Mwajiriwa anaweza kutoa mpango wa pembeni ulio na fidia zilezile kama mpango wa jimbo wa FAMLI na haongezi gharama wala kuweka vikwazo vya vingine. Lazima mipango ya faragha iidhinishwe na Kitengo cha FAMLI.
- Waajiriwa na waajiri wanahimizwa kuripoti ukiukaji wa FAMLI.